## Maswali

1. Yosia alikuwa na umri gani alipokuwa mfalme?
2. Watu wengi waliabudu nini?
3. Yosia aliamua kufanya nini?
4. Yosia alifanya nini kwa Hekalu?
5. Nini ilipatikana kwa Hekalu?
6. Mbona Yosia alifadhaishwa aliposikia yaliyokuwa kwa kitabu?
7. Yosia aliita nani aje Yerusalemu. Alifanya nini?
8. Yosia alifanyaje sanamu na madhabahu?
9. Yosia alifanya karamu gani Yerusalemu?
10. Yosia alikufa namna gani?

## Majibu

1. Yosia alikuwa na miaka 8 alipokuwa mfalme.
2. Watu wengi waliabudu sanamu-Baali na Ashitorethi.
3. Yosia aliamua kwamba atafunza watu wake kumpenda na kumtumika Mungu.
4. Yosia alirekebisha na kutengeneza Hekali.
5. Kitabu kizee cha sheria za Mungu kilipatikana ndani ya Hekalu.
6. Kitabu kilisema kwamba Mungu ataadhibu watu waovu.
7. Yosia aliita viongozi Yerusalemu. Kitabu kilisomwa, Yosia akaahidi kumtii Mungu.
8. Yosia alizifunja madhabahu na akachoma sanamu.
9. Yosia alifanya siku kuu ya Pasaka Yerusalemu.
10. Yosia alienda kupigana na Wamisri. Akajeruhiwa, akarudishwa Yerusalemu kwa gari na akakufia kule.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1    Mwaka wa 2**

# 27 Mfalme Yosia

## Marejeo

2 Wafalme 22:1—2 na 8—13


## Kiini cha somo

Kuonyesha vile Yosia alijaribu kumpenda na kutii Mungu. Aliaribu uovu wote na akafundisha watu kuabudu Mungu kwa njia ipasayo.

## Maneno maalum

1. Yosia + miaka 8 + tumikia Mungu + ngumu.
2. Nguvu + penda + tengeneza hekalu + abudu.
3. Hilkia + kitabu + Yosia + soma + hukumu.
4. Soma + watu wanasikiliza + udhika + haribu sanamu.
5. Siku kuu ya pasaka + sahau + fanya karamu tena.
6. Farao Neko + Yosia auwawa + watu waliomboleza.

**27.1** Yosia alikuwa na miaka 8 wakati baba yake aliuwawa. Alitawaziawa kuwa mfalme alipokuwa na miaka 8. Yosia alikuwa amelelewa kumpenda Mungu. Alitaka kuabudu na kumtii Mungu. Watu wengi waliokuwa wakishauri mfalme waliabudu miungu ya uongo - Baali na Ashtorethi. Ilikuwa vigumu mtoto wa miaka 8 kushindana na watu wa nguvu. Wengi wao waliabudu hii miungu ya uongo. Ni shida kubwa sana ilikuwa kwa kijana Yosia.



**27.2** Yosia alikuwa mdogo sana lakini aliamua kumtumikia Mungu kila wakati. Aliamua kusaidia watu wake. Aliwafundisha kumpenda Mungu. Yosia aliamini Mungu na Mungu alimsaidia ingawaje alikuwa mdogo. Mungu alimsaidia kuwa na nguvu. Yosia alikuwa mmoja wa wafalme bora kwa ufalme wa Yuda. Yosia alitaka kuziharibu sanamu zote. Alitaka kufundisha watu kumtumikia Mungu wa kweli. Kwanza aliamrisha hekalu ya Mungu irekebishwe na kuwa safi. Kwa mda mrefu watu waliabudu sanamu, hekalu haikutumiwa. Ilikuwa chafu na kuharibika. Yosia alirekebisha hekalu ili watu waabudie Mungu.

**27.3** Kuhani Hilkia alipokuwa akitengeneza chumba kimoja kwa hekalu, alipata kitabu kizee sana. Alimuita Shafani mwandishi. Shafani alimsomea hicho kitabu. Hiki kitabu kilikuwa nakala ya sheria za Mungu alizopewa Musa. Inadhaniwa kwamba kilikuwa kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Hilkia aliambia Shafani apelekee mfalme Yosia hicho kitabu na amsomea. Yosia alifurahi alipoona kitabu kilichopatikana kwa hekalu. Yosia alisikiliza kwa makini wakati Shafani aliendelea kumsomea. Kitabu kilinena juu ya adhabu yenye Mungu atatoa kwa watu watakaomuasi. Eti Mungu ataadhibu wanaoabudu sanamu. Yosia alifadhaishwa sana, alijua kwamba watu walikuwa wameabudu sanamu kwa miaka mingi. Walikuwa waovu sana. Yosia aliuliza kuhani Hilkia aombe kwa Mungu. Mungu alimtumia Yosia ujumbe, akimwambia kwamba alikuwa na huzuni kwa sababu watu walikuwa waovu. Lakini Mungu alijua kwamba Yosia alimpenda na alimtumikia. Aliendelea kumwambia kwamba hataadhibu hawa watu wakati Yosia angali mfalme.

**27.4** Aliwakusanya viongozi wote wa mji na vijiji. Aliwaita wote Yerusalemu ili wasikilize yaliyokuwa kitabuni. Kitabu kilisomewa watu wote. Kila mtu alisimama. Yosia aliahidi kwamba watatii sheria za Mungu zote. Yosia alinuia kuharibu sanamu zote zilizoabudiwa. Alitaka kufundisha watu juu ya sheria za Mungu. Alirusha inje madhabahu yote iliyojengewa sanamu huko Yerusalemu. Alichoma hizo sanamu inje ya Yerusalemu pahali panapoitwa Kijito cha Kidroni. Yosia alizunguka Yuda yote. Pote pote alipoenda aliharibu madhabahu na kuchoma sanamu. Alifundisha watu wampende Mungu na kumtumikia.



**27.5** Hicho kitabu kilizungumuzia siku kuu ya Pasaka pia. Mungu aliamurisha watu wawe na siku kuu ya Pasaka kila mwaka. Hiyo siku kuu ya Pasaka iliwakumbusha vile waliokolewa kutoka kwa utumwa Misri. Wote walishukuru na kuabudu Mungu. Yosia alijua watu walikuwa wamesahau kutii siku kuu ya Pasaka. Yosia alikusanya watu wote Yerusalemu ili wawe na siku kuu ya Pasaka. Yosia alifuata amri zote zilizokuwa kwa kitabu. Yosia aliwapa kondoo wakule pamoja na mikate isiyotiwa chachu na mboga zenye uchungu kulingana na vile Mungu aliamuru. Ilikuwa siku kuu ya ajabu Yerusalemu tangu wakati wa Samweli.

**27.6** Farao-Neko, mfalme wa Misri alisafiri na jeshi lake kupita nchi ya Yuda. Alisafiri kwenda kaskazini kupigana na mfalme wa Ashuru. Yosia alikuwa amekatazwa asiwafanyie Wamisri chochote. Lakini Yosia alijaribu kuwapinga Wamisri. Alienda kuwashambulia na jeshi lake. Akapigana nao na akajeruhiwa vitani. Alibebwa kwa gari akarudishwa Yerusalemu na akafa huko. Watu wote waliomboleza kwa kifo cha Yosia. Yosia alikuwa mfalme mzuri sana. Aliamini Mungu, Aliharibu sanamu zilizoabudiwa. Alifundisha watu wakampenda na kumtumikia Mungu. Watu wote wa Yuda waliomboleza kwa sababu ya mfalme Yosia.